

Mafundisho Ya Madhehebu

Mashahidi ya Yehova - 2

Kama tulivyoona juma lililopita kwamba Dhehebu la Mashahidi limeanzishwa na mwanadamu na tena wanakataa mamlaka ya Biblia na kuabudu Chama chao na mafundisho ya chama zaidi ya maandiko. Leo tutaendelea na kuangalia badhi ya mafundisho yao.

Mafundisho Yao:

Chama Cha Watchtower wanafundisha Yesu sio Mungu bali ni malaika aliyeumbwa na Mungu. Pia wanadai Yesu hakufufuliwa na mwili wake na wanadai Yesu ni Mikaeli, mmoja wa hao wakuu wenye cheo, Dan. 10:13.

Mafundisho ya Biblia:

- I. Tunaona Biblia hajawahi kusema Yesu ni Mikaeli au sawa na Mikaeli. Maandiko yanataja Mikaeli mara tano tu katika maandiko na hakuna hata sehemu moja inayoeleza kuwa Yesu ni Mikaeli.
 - A. Dan. 10:13, inaeleza Mikaeli ni moja wa hao wakuu wa mbele.
 - B. Dan. 10:21, inaeleza Mikaeli ni mkuu wa wana wa Israeli.
 - C. Dan. 12:2, Jemadari mkuu, asimamaye upande wa wana wa watu wako (wana wa Israeli).
 - D. Yuda 9, alishindana na Shetani.
 - E. Ufu. 12:7, Mikaeli na malaika zake wakapigana na yule joka, Ufu. 12:7.
 - F. Sasa ni mstari upi kati ya hii unaosema Yesu na Mikaeli ni mtu moja?

- II. Thibitisho zaidi inaonyesha Yesu sio Malaika.
 - A. Yoh. 5:23, tunaona tunatakiwa kumheshimu Yesu kama tunavyoheshimu Baba.
 - B. Ebr. 1:6, Baba ameamuru malaika wote wamwabudu Yesu.
 - C. Yoh. 1:1-3, 7, 14, mwanzoni Yesu alikuwa na Mungu na alikuwa Mungu.
 - D. Yoh. 8:58; Ufu. 1:8; 21:6; 22:13, Yesu hakuumbwa na Baba bali alikuwa Muumbaji.

- III. Maandiko yanaonyesha Yesu ni mtu moja na amefufuka.
 - A. Yoh. 2:19-22, Yesu alisema ata _____?
 - B. Yn. 20:24-28, Yesu alionyesha nini kwa Tomaso? _____
 - C. Zab. 16:10, Daudi alitabiri nini? _____
 - D. Mdo. 2:30-31, Petro alidai nini kuhusu Yesu? _____
 - E. Mdo. 1:1-3, Yesu alikuwa hai au ni mtu mwingine hapa? _____
 - F. Mdo. 1:11; Efe. 4:10; Ebr. 10:12, ni yule yule aliyefufuka au mtu mwingine? _____

- IV. Tujue maandiko yanafundisha kuwa Yesu na Baba ni kitu kimoja.
 - A. Yoh. 1:1-3, 7, 14, Neno alikuwa _____?
 - B. Yoh. 17:5, Yesu alikuwa _____?
 - C. Flp. 2:6, Yesu ni sawa na _____?

D. Pia soma Yn. 14:11 na 17:21.

Hitimisho:

Tumeona kwa majuma mawili ya kuwa Dhehebu la Mashidi Wa Yehova wanafundisha na wanaamini tofauti sana na Biblia. Kwanza wanaheshimu vitabu vyao zaidi ya Biblia. Tena wanakataa Uungu wa Yesu Kristo. Kama Kanisa la Kristo leo tunavyoamini sana Maandiko na Yesu ni Mungu aliyekufa na aliyefufuka kwa ajili ya kila mtu. Kama watu wanapinga Biblia na Yesu ambaye anamamalaka yote hapa ulimwenguni, Mat. 28:18-20, tuachane nao.